AIMWA 008

# WISDOM SERIES

# DARASA LA SITA MUHULA WA TATU

# KISWAHILI

***Jaza nafasi 1-15 katika kifungu hiki kwa kuchagua jibu sahihi.***

Visa vya ujambazi vilikuwa __1__ katika kaya __2__ wanakijiji walikuwa na __3__ yasiyo na kifani. Waliwasilisha matatizo yao kwa chifu aliyeamuru askari washike __4__ usiku __5__. Siku ya __6__, askari waliwashika __7__ wengi ambao walikuwa wakirandaranda usiku. Washukiwa hao __8__ pingu na kupelekwa __9__ katika kituo cha polisi. Siku iliyofuata walipelekwa __10__. Huko walisimama __11__ na kujibu mashtaka __12__ yote na hapo kiongozi wa mashtaka aliwaita mashahidi waliotoa __13__ wao barabara. Hakimu aliwapata na __14__ ya wizi wa __15__ na kuamuru watiwe kitanzi. Lilikuwa funzo kwa wengi na visa vya wizi vikaisha kabisa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | vimeisha | vimekithiri | vimepotea | vimedidimia |
| 2. | wetu | petu | letu | yetu |
| 3. | masahibu | maswahiba | masaibu | mashaibu |
| 4. | Wahalifu | wezi | hatamu | doria |
| 5. | kutwa | kuta | kucha | kuchwa |
| 6. | kwansa | kuanzwa | kwanza | kuanza |
| 7. | watuhumiwa | majambazi | wahalifu | wezi |
| 8. | walijivalisha | walizivaa | walibanwa | walivaa |
| 9. | gerezani | korokoroni | seli | rumande |
| 10. | jela | kortini | kotini | mahakamani |
| 11. | kizimbani | mimbariri | kirimbani | jukwani |
| 12. | waliikia | walilenga | walikiri | walikanusha |
| 13. | ushahidi | malalamishi | ushuhuda | ujuzi |
| 14. | uhuru | hatia | hatua | masaibu |
| 15. | mdogomdogo | mzuri | uchopozi | mabavu |

***Kutoka swali la 16 hadi 30 chagua jibu sahihi.***

16. Kamilisha methali:- Ngoja ngoja________
    A. atakuja
    B. upate chakula
    C. hana baraka
    D. huumiza matumbo

17. Ni neno lipi kati ya haya halipatikani katika ngeli ya A-WA?
    A. Kiziwi B. Kuku
    C. Mvua D. Paka

18. Kinyume cha mchana ni ___________

A. usiku B. asubuhi

C. jioni D. adhuhuri

19. Sehemu ya ndani ya vidole vya mkono huitwa:-

A. kiganja B. kisigino

C. kiganja D. paja

20. Baba yangu alipigiwa simu na ndugu yangu jana. Neno pigiwa liko katikia ngeli ya _______

A. kutendeka B. kutendea

C. kutendesha D. kutendewa

21. Tumia "amba" Kalamu ___ imenunulia ni nzuri.

A. ambazo B. ambaye

C. ambalo D. ambayo

22. Wanyama wote walitega masikio _________

A. Ji B. Ndi

C. Tye D. Zi

23. Ukizidisha nusu na thuluthi utapata:-

A. sudusi B. tusui

C. thumuni D. sudusi tano

24. Utajibuje ukiambiwa waambaje?

A. vyema

B. vibaya

C. vizuri

D. sina la kuamba

25. Andika kwa wingi:- Karatasi imeraruka.

A. Makaratasi yameraruka

B. Karatasi zimeraruka

C. Makaratasi zimeraruka

D. Karatasi imeraruka

26. Kiluwiluwi ni kwa chura kama vile _________ ni kwa ndovu.

A. ndama B. kibuli

C. shibli D. kiyoyo

27. Humu _________ nyanya yumo.

A. ndilo B. ndimo

C. ndiko D. ndipo

28. Maana ya kufa moyo ni ___________

A. kuugua moyo

B. moyo kusimama

C. kuaga dunia

D. kukosa matumaini

29. Ni sentensi ipi iliyo sahihi:-

A. Mifugo mingi imefungwa

B. Nyumba huu umepambwa

C. Jino langu imeng'oka

D. Miti mingi imekatwa

30. Mwana wa kwanza kuzaliwa tunamwita:-

A. kikwanza

B. tangulizi

C. kitinda mimba

D. kifungua mimba

***<u>Soma shairi hili kisha ujibu maswali 31-40.</u>***

Waswahili ndugu zangu, nina mzo ya kusema,
Ambayo yana uchungu, fuasi yananiuma,
Yanigonga ya kiningu, naumwa mwili mzima,
Hizi simu za mikono, jamani zina vioja.

Waumini wakiomba, na kusali kanisani,
Simu toka kwa mjomba, na inalia mkononi,
Wapiga ukijigamba, humheshimu manani,
Hizi simu za mikono, jamani zina vioja.

Usikani ukishika, dereva ninakwambia,
Madaraja unavuka, mbio simu ikilia,
Watu roho zawatoka, ajalini kutokea,
Hizi simu za mikono, jamani zina vioja.

Wanafunzi ni mabunga, hawashiki ya mwalimu,
Wameshinda kujinyanga, kubonyeza dude simu,
Wakifunga na kufunga, wamekosa ya muhimu,
Hizi simu za mikono, jamani zina vioja.

Nimehimili mawimbi, nikatua ufuoni,
Nimeonya sakubimbi, kuyatia maanani,
Litakuwa jema ombi, tukizima majinuni,
Hizi simu za mikono, jamani zina vioja.

31. Wanafunzi mabunga ni wanafunzi wapi?
A. Wanaoshinda kwa kupiga simu wakati wote
B. Waliotufunza darasani
C. Wasioelewa mambo sawa na wapumbavu
D. Watukutu wasiowatii walimu wao

32. Shairi aina hii lenye mishororo minne huitwaje?
A. unne B. tasdisa
C. takhmisa D. utungo

33. Shairi linaonya kina nani?
A. Wapigiwao simu
B. Waswahili wote wazungumzao na ndugu zao
C. Wanaomiliki rununu
D. Waumini

34. Kulingana na maoni ya malenga:-
A. anawakanya watunzao simu ipasavyo
B. anawaasa na kuwasua watumiao simu za mikono
C. hana simu wala hawasiliani na yeyote
D. haoni umuhimu wa matumizi ya simu

35. Taja vina vya kati katika ubeti wa mwisho:-
A. ni B. mbi C. i D. bi

36. Sheria za utunzi wa mashairi huitwa:-
A. vina B. arudhi
C. mizani D. mbinu

37. "Hizi simu za mikono jamani zina vioja."
Mshororo huu ni:-
A. tarbia B. kibwagizo
C. kina D. ubeti

38. Malenga ni kwa utunzi naye Manju ni kwa:-
A. Uhifadhi B. Ukosoaji
C. Usomi D. Ughani

39. Shairi hili lina beti ngapi?
A. Nne B. Sita
C. Tano D. Tatu

40. Shairi hili lina mishororo mingapi kwa jumla?
A. 16 B. 20
C. 25 D. 4

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 41-50.***

Ukosefu wa kazi kwa vijana unachangia umasikini mkubwa katika taifa nzima. Idadi kubwa ya vijana hushinda kutwa nzima bila kufanya lolote wala chochote. Hali hii huchangia kuzorota kwa uhusiano wa kijamii wizi na hata utumiaji wa dawa za kulevya. Uchumi wa nchi hurudi nyuma na taifa huwa ovyo. Huku shida hii ikizidi **kupamba moto** bei ya bidhaa muhimu kama vile mafuta, unga, mahindi, na mchele inazidi kupanda kila uchao.

Mazao yanapungua kutokana na ukosefu wa mvua. Serikali imekuwa imenyamaza kimya licha ya kuwa wananchi wanaaga dunia kutokana na njaa. Mkoa wa kazkazini mashariki ndio umeathirika sana. Watoto katika mkoa huu hawahudhuri masomo kutokana na njaa, hali ambayo imechangia pia kuzorota kwa masomo nchini. Hali hii ya kuzorota kwa masomo inapopita mipaka, walimu ndio hulaumiwa na wakati mwingine kutishiwa kupigwa kalamu.

Ikiwa serikali haitajikakamua na kushughulikia swala hili basi taifa litaangamia na waja watazidi kuaga dunia. Lakini afueni ipo kwani waziri wa fedha ametangaza kuwepo kwa mpango wa kuwapa maskini pamoja na vijana msaada wa pesa ambao utawawezesha kuanzisha biashara ili kujikimu katika aushi yao. Mpango huu wa kuwapa waathiriwa msaada unaonyesha nia njema ya serikali na ikiwa basi serikali inaendeleza juhudi hizi za kupigana na ukosefu wa ajira na njaa basi sote tutajivunia kuwa wananchi wa taifa letu.

41. Neno taifa kama lilivyotumika katika makala haya linapatikana katika ngeli gani?

A. I-ZI

B. I-I

C. YA-YA

D. LI-YA

42. Ni lipi ambalo halileltwi na hali ya umaskini na ukosefu wa kazi dhidi ya vijana?

A. Wizi

B. Matumizi ya dawa za kulevya

C. Walimu kupigwa kalamu

D. Kuzorota kwa uhusiano

43. Masomo yanapodorora kutokana na sifa za njaa walimu wanatishiwa kwa nini?

A. Kunyang'nywa kalamu

B. Kuwekewa mipaka

C. Kuhamishwa katika shule zao

D. Kufutwa kazi

44. Ni nini ambacho kimetajwa cha kuwapa maskini na vijana matumaini katika maisha yao?

A. Serikali kuwaajiri vijana

B. Mpango wa kuwapa vijana na maskini msaada wa pesa

C. Kuwepo kwa mvua ya kukuza mazao

D. Waziri wa fedha kuwapa vijana kazi katika wizara yake

45. Kulingana na kifungu umaskini unachangiwa na nini hasa?

A. Vijana kukosa kazi

B. Kuzorota kwa uhusiano wa kijamii

C. Serikali kutowajibika

D. Vijana kukataa kazi

46. Ni hali ipi ya anga ambayo imetajwa kuleta uhaba wa mazao?

A. Hali duni ya mkoa wa Kazkazini Mashariki

B. Watu kuaga dunia

C. Kuepo kwa mvua kubwa

D. Ukosefu wa mvua

47. Kuaga dunia kama ilivyotumika katika habari ina maana gani?

A. Kufa

B. Kuwa maskini

C. Kukosa raha

D. Kuteseka

48. Kifungu "kupamba moto" kilivyotumika katika makala ni fani gani katika lugha?

A. Tashbihi

B. Msemo

C. Methali

D. Kitendawili

49. Kulingana na habari uliyoisoma ni kweli serikali inashughulikia maskini na vijana?

A. La hasha

B. Hatujui

C. Ndio

D. Hatujaambiwa

50. Ni nini kichwa cha habari hii?

A. Mvua duni

B. Ukosefu wa ajira

C. Taifa maskini

D. Ukaidi wa vijana